

WAPAKWA MAFUTA WA UONGO

Mt. Matayo 24:24-25

Kwa maana watatokea makristo wa uongo, na manabii wa uongo nao watatoa ishara kubwa na maajabu; wapate kuwapoteza, kama yamkini, hata walio wateule. Tazama nimekwisha kuwaonya mbele”

Hebu tusikilize kile Nabii wa Mungu alichozungumza:....(Angalia vikaatasi).....

Nawatakeni muone hapa katika Mathayo 24, Yesu alitumia neno “Makristo”, M-a-k-r-i-s-t-o, “Makristo.” Si kristo, bali makristo wingi sio umoja kwa hiyo neno Kristo maana yake ni “Yeye aliyeitwa mafuta.” Ndipo basi iwapo ni “kutiwa mafuta,” hakutakuwa tu na mmoja tu, bali wengi, waliotiwa mafuta, “waliotiwa mafuta.” Mnaona?

La sivyo, kama yeye angetaka kulichambua ili kwa namna fulani tupate kulifahamu vizuri zaidi, yeye angesema, “katika siku za mwisho watainuka waliotiwa mafuta wa uongo.” Naam, hilo linaonekana karibu haliwezekani, naona, hilo neno “kutiwa mafuta.”Bali angalia maneno yanayofuata, “ na Manabii wa uongo, “ m-a-n-a-b-i-i wingi.

Naam, aliyetiwa mafuta, ni, “mtu mwenye ujumbe.”Na jinsi tu ujumbe unavyoweza kuhubiriwa ni kwa mtu ambaye ametiwa mafuta, na huyo angekuwa ni nabii, aliyetiwa mafuta. “watatokea waalimu wa uongo waliotiwa mafuta.”nabii. Hufundisha jinsi ujumbe wake ulivyo. Waalimu waliotiwa mafuta, bali watu waliotiwa mafuta walio na mafundisho ya uongo. Waliotiwa mafuta, “makristo” wingi; “manabii,” wingi. Na kama kuna kitu kama Kri-Kristo, umoja, bali hawa hawana budi kuwa “waliotiwa mafuta,” kwamba unabii wa yale waliyokuwa wanafundisha ndio ungekuwa ni tofauti, kwa maana wao ni waliotiwa mafuta, waliotiwa mafuta.

Naam, ni somo la Jumapili, tunataka ku – kujaribu kuleta jambo hili kwenye shindano halisi la kuamua, kwa maandiko si kwa yale mtu mwingine amesema juu yake, lakini kwa kuyasoma maandiko tu.

Unaweza kusema, “Hii inawezekanaje kuwa? Hivi waliotiwa mafuta.....”

Wao walikuwa nini? “Makristo,” M-a-k-r-i-s-t-o” waliotiwa mafuta. “Makristo, na manabii wa uongo.” Waliotiwa mafuta, bali ni manabii wa uongo!

Yesu alisema ya kwamba, “mvua huwanyeshea wenye haki na wasio haki.”

Naam, mtu fulani aweza akaniambia, “Hivi unaamini ya kwamba huko kutiwa mafuta juu ya watu hao kunamaanisha ya kwamba ni upako wa Roho Mtakatifu? “Naam, bwana, Roho Mtakatifu halisi wa Mungu juu ya mtu, na hata hivyo wao ni wa uongo.

Sasa sikiliza kwa makini uone yale aliyosema. “ Nao watatoa ishara na maajabu, wapate kuwapoteza hata walioteuliwa kama yamkini. “ Nao wanatiwa mafuta kwa Roho Mtakatifu halisi. Najua jambo hili linasikika la kijinga sana, bali tutachukua wakati na kuleleza kwa Neno, ya kwamba hiyo ni kweli kabisa, BWANA ASEMA HIVI.

Kumbuka Biblia ilisema, “katika siku za mwisho watatokea makristo wa uongo” siyo wa Yesu wa uongo. Hilo hawataweza kulistahimili. Lakini makristo wa uongo; wapakwa mafuta wa uongo. Kwa hakika kabisa wamepakwa mafuta na Roho, pamoja na Roho Mtakatifu, na bado ni uongo.

Kuna watu watatu ndani yako, nje ni mwili. Una hisia tano za kuwasiliana na makao yako ya duniani. Na ndani ni Roho na pale kuna hisi tano upendo, na ufahamu wa jema na baya, na kadhalika lakini ndani ya hapo ni Nafsi.

Kumbuka, mvua hunyesha kwa wema na wabaya. Mvua ile ile inayofanya mbegu ya ngano ikue, inafanya gugu nalo likuwe pia unaona? Ni nini? Ndani ya ile mbegu kuna asili na ile inajidhihirisha

yenyewe. Vitasimama katika shamba moja pale pamoja na magugu. Magugu na ngano vimesimama pamoja katika shamba moja, vyote vikifurahi. Vichwa vimeinama chini, vinakuja kwa kukosa maji. Wakati mvua inapokuja, gugu linaweza kupiga kelele kama vile tu ngano iwezavyo kufanya. Lakini kwa matunda yao mtawatambua hao (matayo 7:15-20)

Wakristo, ninaweza nisiwaone ninyi tena tunaweza tusionane tena kaa sawa na Neno la Mungu, Angalia kwenye kioo unaonaje kwenye kioo cha Mungu? Je kinaonyesha sura ya Binti na mwana wa Mungu?

Na sasa, kutakuwa na wapakwa mafuta wa uongo katika siku za mwisho, siyo Yesu wa uongo; hawataweza kusimamia hilo. Lakini wapakwa mafuta wa uongo. Wamepakwa mafuta ndiyo, Bwana, lakini ni wapinga kristo. Wamepakwa mafuta na Roho kufanya ishara na maajabu/miujiza ambayo kristo alifanya, lakini hawatakubaliana na Neno unaona? “Wengi watakuja kwangu siku ile na kusema, Bwana hatukutoa unabii na kutoa pepo kwa jina lako?”

Naye atasema, ondokeni kwangu, ninyi mtendao maovu, sikuwajua kamwe” Nilikuwa Mpentekoste, Bwana utukufu kwa Mungu. Nilipiga makelele, Nilizungumza kwa lugha; Niliweka mikono juu ya wagonjwa na wakaonywa, nilitoa pepo. Ondokeni kwangu, ninyi mtendao maovu kamwe sikuwajua” unaona ninachomaanisha? (Matayo 7:21-23)

Utaratibu wa madhehebu umekufa. Haupo. Hautaamka tena kamwe. Utachomwa moto. Hicho ndicho unachofanya na makapi huko shambani. Kimbia kutoka huko. Ingia ndani ya Kristo, usiseme, “Mimi ni wa Methodist, Mimi ni wa baptisti, mimi ni wa Pentekoste” ingia ndani ya Kristo.

Kama wewe uko ndani ya Kristo, hakuna Neno lililoandikwa ndani hapa usiloliamini. Sijali chochote ambacho mtu mwingine yeyote amesema. Na ndipo Mungu anafanya kitu hicho kudhihirisha. Sababu wewe, wakati Yeye anapomwaga Roho juu ya Neno, kitu gani kinatokea? Kama tu kuweka maji juu ya mbegu nyingine yoyote. Itaishi na itazaa kwa namna yake.

Unasema “mimi nina ubatizo wa Roho Mtakatifu. Hivyo haimaanishi kuwa umeokoka, siyo hata kwa mbali.

Tazama hapa. Wewe u kiumbe wa utatu. Ndivyo ulivyo. Ndani katika jamaa huyu hapa pana nafsi, baada ya hapo Roho, baada ya hapo mwili. Sasa una hisi tano katika mwili ili kuwasiliana na nyumbani kwako hapa duniani. Hizo haziwasiliani na vinginevyo isipokuwa hivyo. Unazo hisi tano za Roho, hapa: upendo, dhamiri na kadhalika, za hiyo, lakini ndani hapa ndimo unamoishi. Hicho ndicho wewe ulicho.

Je, Yesu hakusema “Mvua huwanyeshea wenye haki na wasio haki? [kusanyiko linasema – “Amina” – Mh] uweke gugu nje hapa, na ngano nje pale, na umwagilie zote maji, na uwekee zote mbolea, na vitu kama hivyo, je vyote viwili havitaishi kwa maji yale yale? [“Amina] Hakika. Vema, hicho ni kitu gani? Mojawapo itazaa gugu, kwa sababu hicho ndicho lilicho. Gugu litainua mikono juu na kupiga kelele vile vile kama ngano itakavyofanya.

Je, Biblia haisemi. “katika siku za mwisho kutotokea Makristo wa uongo [kusanyiko linasema, Amina” – Mh] siyo “Yesu wa uongo”, sasa.

“Makristo wa uongo” watiwa mafuta, wanaolijia Neno wakiwa watiwa mafuta wa uongo; waliotiwa mafuta ya kidhehebu, lakini siyo ili kulijia Neno.

Kwani Neno litajishuhudia lenyewe. Halihitaji kitu kingine chochote. Litajishuhudia lenyewe. “Na watatokea watiwa mafuta wa uongo.” Mnayo kanda yangu niliyohubiri juu ya hilo. Na yule mtiwa.....

Aa, ungelimwita mmojawapo, useme. Aaa, wewe Yesu fulani? “Aa, hakika, hapana”. Hawawezi kusimamia hilo.

Lakini inapofikia pale “ Au utukufu” !Ninao upako. Kumbuka kayafa alikuwa nao, pia, na akatabiri.

Lakini hilo halihusiani na chochote na hili, kwa ndani. Labda iwe kwamba huyo alikuwa mbegu ya Mungu, chembe kutoka mwanzo,

sijali unapiga kelele kiasi gani, unanena kwa lugha kiasi gani, unakimbia, unapiga kelele. Hilo halihusiani chochote na hili.

Gugu laweza kuwa na hali zote, mazao mengine yaliyo nayo. Mimi nimeona makafiri wakisimama, na kupiga makelele, na kunena kwa lugha na – na kunywa damu toka kwenye fuvu la kichwa cha mwanadamu na kumwitia Shetani. Manaona? Hivyo usi.....Mojawapo ya hisia na vitu kama hivyo, sahau hilo.

Ni moyo wako katika hilo Neno, na huo ni Kristo. Ilete ndani pale, na itazame ikijifanya yenyewe kufahamika, wakati inapofunguka tu kama mbegu nyingine yoyote, na kujitangaza yenyewe katika kipindi inachoishia ndani yake.

Luther hakuleta chochote isipokuwa kitawi. Hawa wengine waliweza hivi vitu vingine. Sasa tupo katika kipindi cha ngano.

Akina Luther wa Luther ilibidi wamlete Luther halisi Pentekoste halisi ilipasa ilete pentekoste halisi. Ndivyo hivyo. Lakini tumekwisha pita kipindi hicho, na tunaendelea mbele.

Kama ilivyokuwa kwenye ujumbe wangu kuhusu mpinga Kristo. “Watainuka makristo wa uongo” sasa hakusema mayesu wa uongo unaona hakuna ambaye angestahimili hilo la kuitwa “Yesu” ikimaanisha Bwana. Lakini makristo wa uongo yamaanisha “wapakwa mafuta” oh kila mmoja

anafikiri kwamba ana upako wa mafuta, utukufu kwa Mungu, anaweza kufanya hivi na kufanya vile. Lakini muweke kwenye kipimo cha Neno – na umuone anatokea wapi, katika ujumbe wa saa walikuwa na upako wakati wa Yesu, lakini haikuwa kwake. Walikuwa na upako wakati waDathon alikuwa na upako wakati wa Musa Alisema, sasa usifikiri ni wewe tu uliye mtakatifu miongoni mwetu; Mungu anao wengi. Tutaanzisha tu chama hapa, kundi la wanaume (Hesabu 16:1-35)

Mungu akamwambia Musa, “Jitenge kati yao” Aliifungua dunia ikawameza alilitoa Neno lake la asili kumpa Musa, Nabii wake; hiyo

ndiyo; hiyo ndiyo njia pekee aliyoitumia, na njia pekee awezayo kulifanya hilo. Habadilishi mpango wake. Unaona?

Sikiliza yeye alisema, “wale wasioweza kustahimili kurudiwa ni wana haramu wala si wana wa Mungu.” Mwaona, wao waliwashwa-washwa tu. Mwaona, ile mbegu niliyonena habari zake muda mfupi uliopita, nafsi hiyo haikuweko kwanza. Ilikuwa na upako wa Roho, naye akatenda mambo mbalimbali. Lo, wewe na hao....na wakati Roho yako ina upako, unaweza ni Roho Mtakatifu halisi na wakweli hata hivyo ungeweza tu kuwa ibilisi.

“Lo” unasema, “Ndugu Branham!”

Manabii wa uongo! Biblia ilisema, “Katika siku za mwisho kutakuweko na manabii wa uongo.” Yesu alisema, “Watatokea makristo wa uongo.” Si “Ma-Yesu wa uongo,” Sasa, hamna anayeweza kuvumilia hayo; bali “makristo wa uongo” Kristo maana yake ni “walio na upako” Walio na upako na niwatiwa mafuta wa uongo; wao wana upako, bali chanzo chao ni uongo, nao wanatenda ishara nyingi na maajabu, wananena kwa lugha, wakacheza kwa Roho, wanahubiri Injili.

Yuda Iskariote alifanya hayo! Simeoni....au la, samahani....Kaiyafa alitabiri! Balaamu, yule mnaifi! Bila shaka, akafanya ishara zote, kila kitu, Matendo yote ya kidini.

Lakini, Mwaona, ukipanda punje ya gugu na punje ya ngano katika tuta lile lile na kuzimwagilia maji na kuzinyunyizia, zote mbili zitafurahi. Zote mbili zitachipuka kwayo, maji yale yale. “Jua huwaangazia wenye haki na wasio haki na mvua huwanyeshea wenye haki na wasio haki, bali kwa matunda yao mtawatambua.” Unawezaje kutoambatana na Neno? Amina. Mnaona ninayomaanisha? Maji huwamwagikia wenye haki na wasio haki, kuwanyunyizia.

Yesu alisema, Watakuja kwangu siku ile, wakisema, ‘Bwana! Bwana! Sikutoa pepo? Sitakutabiri? Sikufanya mambo makuu katika jina lako? Yeye atasema, “Ninyi mtendao maovu, ondokeni kwangu, hata siwajui. Enendeni kwenye kuzimu kwa milele alikowekewa tayari Ibilisi na malaika zake.” Mnaona? Ni Neno jinsi gani! Wa uongo. Huabudu bure, hujitahidi bure. Mbona mnaofanya hivyo na huku

haiwapasi kufanya hivyo? Mbona mchukue mwigizo na humu mbingu zimejaa yaliyo halisi? Mwaona? Haiwapasi kufanya hivyo.

Sasa linganisha hayo na Mathayo 5:24 tena. Angalia Yesu alisema mvua na jua huja juu ya nchi, ya kwamba Mungu huituma kutayarisha chakula na vinginevyo kwa ajili ya watu wa duniani. Nayo mvua hutumwa kwa ajili ya chakula, mboga. Bali magugu, kwekwe, vikiwa mashambani, hupokea kitu kile kile. Mvua ile ile inayoifanya ngano kukua ndiyo mvua ile ile inayoyofanya kwekwe kukua.

Jinsi nilivyokuwa na somo juu ya jambo hilo wakati mmoja, wakati nilipokutana na Wapentekoste kwa mara ya kwanza! Nalo lilikuwa somo kubwa kwangu. Niliwaona watu wawili, mmoja....sikuwa nimewahi kusikia kunena kwa lugha hapo kabla. Mmoja alinena kwa lugha, huyo mwingine akaifasiri, na huyo mwingine vivyo. Nao wangesema kweli, wakasema kwamba, “Kuna wengi hapa wanaopaswa kutubu usiku huu. Kuna wanawake na wanaume, wote wawili.” Nao hao watu wangesimama waende madhabahuni.

Nikawaza, “Ni la utukufu jinsi gani!”

Ndipo nikiwa na kile kipawa kidogo cha Roho Mtakatifu nilizungumza na watu hao, tu mwajua jinsi gani, katika upambuzi, kidogo tu nipate kujua. Na moja wao alikuwa Mkristo halisi, naye alikuwa mtumishi halisi wa Kristo, na huyo mwingine alikuwa mnafiki. Na mmoja wao, huyo aliyekuwa mnafiki, alikuwa anaishi na mwanamke mwenye nywele nyeusi, huku anazurura na mwanamke mwenye nywele za shaba na alikuwa amezaa watoto naye. Vema, lilikuwa pale kwenye ono; halingeweza kukanushwa. Nami nikazunguka kwenye lile jengo.

Sasa nilikuwa nimechanganyikiwa, bila shaka. Nilifikiri nilikuwa nimekutana na malaika, kasha nikashangaa kama sikuwa kati ya pepo. Hii ingewezekanaje? Mimi sikuweza kuelewa na jambo hilo. Na kwa miaka mingi nikajiepusha nalo, mpaka siku moja wakati.....

George Smith, yule mvulana anayetembea na binti yangu, tulienda jana huko kwenye kinu cha kale ambako mimi huenda kuomba.

Na baada ya kuwemo mle ndani siku kadha, Roho Mtakatifu akaniletea andiko hili. :” Kwa maana mvua hunyeshea mara kwa mara na kuzaa mboga, bali michongoma na miiba huishi kwa mvua ile ile, ambayo mwisho wake ni kuteketezwa. “Vikiishi kwa chemchem ile ile itoayo uzima ya Mungu. Ndipo nikafahamu hilo. “Kwa....” Yesu alisema, “kwa matunda yao wana tambulikana.”

Naam, kwa hiyo mvua ikishuka juu uoto wa asili wa nchi, ni mfano wa mvua ya Kiroho ambayo inatoa Uzima wa Milele, ikishuka juu ya Kanisa, kwa kuwa tunaiita mvua za masika na mvua za vuli. Na ni mvua, ikimwagika kutoka kwa Roho wa Mungu, juu ya Kanisa lake.

Angalia, ni jambo la ajabu sana hapa. Mnaona? Wakati hizo mbegu zilipoingia ardhini, haidhuru ziliingiaje mle, zilikuwa michongoma kwanza. Lakini hapo ngano ile ambayo iliingia ardhini, na mboga, zilikuwa mboga kwanza. Na kila mboga ikijizaa yenyewe, tena, inaonyesha ya kwamba ilikuwapo katika mwanzo wa asili.

“Nao watawapoteza walioteuliwa kama yamkini,”maana wao wanapata mvua ile ile, baraka zile zile, wakionyesha ishara zile zile, maajabu yale yale. Mnaona? “Wao watawapoteza, ama watawapoteza walioteuliwa kama yamkini.” Naam, mchongoma hauwezi kujizuia kuwa mchongoma, wala ngano haiwezi kujizuia kuwa ngano; ni kile Muumba wa kila mmoja alichokusudia hapo mwanzo. Hao ni wale walioteuliwa. Mvua ile ile!

Jua huchomoza asubuhi na kuenea kila mahali duniani, kama ilivyofanya dunia hii na siku hii tunayoishi. Nalo jua, jua lile lile linalochomoza mashariki ndilo jua lile lile linalotua magharibi. Na jua hilo linatumwa kuivisha punje juu ya nchi, ambazo miili yetu imefanywa kwazo.

Tunaishi kwa vitu vilivyokufa. Hiyo ndiyo njia pekee unayoweza kuishi. Na iwapo kitu fulani hakina budi kufa kila siku ili upate kuishi, kwa kawaida, je! Basi si ni kweli kwamba kama nini yako.....Mwili wako hauna budi kuishi kwa vitu vilivyokufa, kwa ajili ya maisha ya kawaida, basi huna budi kuua kitu fulani, kiroho, kuyaokoa maisha yako ya kiroho. Naye Mungu. Alifanyika mwili, nyama, kisha akafa tupate kuishi. Hakuna kanisa, hakuna kitu kingine

ulimwenguni kinachoweza kukuokoa ila Mungu. Hicho ndicho kitu pekee wanachoishi kwacho.

Lakini unaona, “Yeye huituma mvua,”tulirudie somo letu, “kwa wenye haki na wasio haki.” Yesu anawaambia jambo hilo hapa sasa, katika Mathayo 24, ingekuwa ni ishara wakati wa mwisho.

Naam, iwapo ishara hii itajulikana tu katika wakati wa mwisho, basi haina budi kuwa ni baada ya kufunuliwa kwa Muhuri zile. Mnaona? Ni ishara ya wakati wa mwisho. Hiyo ingekuwa, wakati wa mambo haya yatakapotukia, itakuwa kwenye wakati wa mwisho. Na itakuwa ni ishara, sasa, ili kwamba walioteuliwa wasichanganyikiwe katika mambo haya. Mnaliona? Basi, haina budi kufunuliwa, kuonyeshwa wazi.

Angalia, vyote viwili ngano na magugu huishi kwa upako ule ule utokao Mbinguni. Vyote viwili hufurahia juu yake.

Ninakumbuka jambo hili, nikirejea kwa kisa hiki hapa siku ile kwenye kinu cha Green. Ni – niliona hilo ono likitukia. Na kulikuwa na dunia kubwa, na yote ilikuwa imelimwa. Ndipo akatokea Mpanzi, kwanza. Nataka kuweka hilo mbele yenu. Angalia kinachotokea kwanza, halafu kinachofuata. Na hapo Mtu huyu mwenye vazi jeupe alipotokea kuizunguka dunia, akipanda mbegu, kasha nyuma yake akaja mtu, amealia nguo nyeusi, alionekana mjanja sana, akinyemelea nyuma yake, anapanda magugu. Na wakati jambo hili lilipotukia, ndipo nikaona mimea yote miwili ikimea. Na ilipokuwa inamea, mmoja ulikuwa ni ngano, na mwingine ulikuwa ni magugu.

Kisha kukatokea ukame, hapo ambapo ilionekana kana kwamba, yote miwili ilikuwa imeviinamisha vichwa vyao ikililia mvua. Ndipo likatokea wingu kubwa juu ya nchi, halafu mvua ikanyesha. Ndipo ngano ikainuka na kusema, “Bwana asifiwe! Bwana asifiwe! “ Nayo magugu yakainuka na kupiga kelele, “Bwana asifiwe! Bwana asifiwe! “Matokeo yale yale. Yote miwili ikiangamia, yote miwili ikiondoka. Kisha ngano inainuka na kuona kiu. Na kwa sababu ilikuwa katika shamba lile lile, bustani ile ile, mahali pale pale, chini ya bubujiko lile lile la maji, ngano ikainuka kisha magugu yakainuka kwa kitu kile

kile. Angalia, maji yale yale yenye upako yanayootesha ngano, huotesha magugu.

Roho mtakatifu yule yule anayelitia kanisa mafuta; ambaye anawapa shauku ya kuwaokoa watu, anayewapa nguvu za kufanya miujiza, anawashukia wasio haki sawasawa na wenye haki. Roho yule yule! Naam, huwezi kuifanya namna nyingine na ufahamu Mathayo 24:24. Yeye alisema, “Watatokea makristo wa uongo,” uongo, waliotiwa mafuta. Waliotiwa mafuta kwa kitu kilicho halisi, bali wawe manabii wa uongo wa kitu hicho, waalimu wa uongo wa kitu hicho.

Ni nini kingemfanya mtu atake kuwa mwalimu wa uongo kwa kitu kilicho kweli? Sasa tutafikia ile alama ya mnyama waalimu wa uongo; wa uongo, wametiwa mafuta. Makristo waliotiwa mafuta, bali ni waalimu wa uongo. Ndiyo njia pekee.

Loo, enyi waalimu wa uongo mliosikiza kanda hizi miaka hii yote, na kuona Mungu akithibitisha yale hasa aliyosema, na mnaketi katika vyumba vyenu vya kusomea na kujua ya kwamba ni kweli; na kwa sababu ya tofauti zenu za kimadhehebu, mnaupinga na kuwaambia watu wenu si kweli. Ole wenu! Wakati wenu umekaribia.

Balaamu, aliyetiwa mafuta kwa roho yule yule aliyekuwa juu ya Musa. Tofauti ilikuwa ni nini? Mafundisho ya Musa yalikuwa makamilifu. Biblia ilisema hapa katika petro wa pili, ya kwamba ilikuwa ni “mafundisho ya balaamu” ambayo Israel walipokea, ambayo Mungu kamwe hakusamehe. Dhambi isiyosameheka! Hakuna hata mmoja wao aliyeokolewa, hata ingawa walikuwa wamekuja chini ya baraka za Mungu. Na, kwa sababu, nabii mwingine aliingia na mafundisho fulani, kinyume na kumpinga Musa, na kujaribu kuwathibitishia watu ya kwamba Musa alikuwa amekosea. Naye Dathan, Korah, na wengine wengi, walikubaliana naye na kuwafundisha wana wa Israel kufanya uasherati, kuyafuata madhehebu yake, ya kwamba, “sisi sote tu kitu kimoja”.

“Kama sisi ni Wamethodisti, wabatisti, wapresbiteri, ama wapentekoste, na chochote kile sisi ni kitu kimoja”

Sisi si kitu kimoja! Sisi ni watu waliotengwa, watu watakatifu kwa Bwana, waliowekwa wakfu kwa Neno na Roho wa Mungu, kuzaa tunda la ahadi yake ya siku hii. Nawe si mmoja wao! Najua hilo ni kali sana, bali hiyo ni kweli haidhuru. Waliowekwa wakfu kwa ajili ya utumishi katika siku hizi za mwisho! “Tokeni kati yao.”

Naam, “Mafundisho ya Balaamu,” si unabii wa Balaamu. Huo ulikuwa sawa. Huyu alikuwa ni Mungu. Ni wangapi wanaoamini jambo hilo? [kusanyiko linasema, “Amina.” – M] unabii wa balaamu ulikuwa sawa kabisa, maana yeye asingeweza kunena lingine. Upako wa Mungu usingelinena kitu kingine chochote, naye Mungu aliuhakikisha kwa kuthibitisha ulikuwa kweli. Lakini “mafundisho ya Balaamu”.

Sasa linganisha hilo na Mathayo 24:24.

Sasa, ninyi ni kusanyiko. Naam, ni nani aliyesahihi? Wote wawili ni manabii. wote wawili ni manabii. Jinsi tu unavyoweza kujua tofauti kati yao, ni kulichunguza kwa neno. Usikose kuupata ujumbe huu.

Kila ishara, kila ajabu, mtu aliyetiwa mafuta, unabii, kila aina ya mambo yanayoendelea; aina zote za ishara aina zote za maajabu, utajuaje tofauti yake? Angalia Neno la wakati huu. Roho Mtakatifu ndiye Nabii wa saa hii wakati huu. Analidhibitisha Neno lake; analihakikisha. Roho Mtakatifu alikuwa ndiye Nabii wa wakati wa Musa. Roho Mtakatifu alikuwa Nabii wa wakati wa mikaya Roho Mtakatifu aliandika Neno, anakuja na kulithibitisha Neno.

Oh, enyi waalimu wa uongo, ndivyo anavyosema Mungu siku moja mtavuna mnayopanda, enyi viongozi vipofu wa vipofu! Sina hasira. Ninawaambieni kweli tu. Na nisingelisema jambo hili kama hapa, kwenye kile chumba, kama Roho Mtakatifu hakusema. “liseme kwa jinsi hiyo” Je nimepata kuwaambia jambo lolote lisilo kweli ila lile Mungu alilolithibitisha kuwa ni kweli? Amkeni, ndugu, ndugu zangu kabla ya kucheleva sana.

Bali hebu niseme jambo hili. Mwiba ungewezaje kuamka kisha uwe mchongoma, wakati ulikusudiwa tangu zamani kuwa hivyo? Wateule wangepata kutoliona? Kwa sababu wao wamechaguliwa kuliona,

wote alionipa Baba watakuja kwangu”, alisema Yesu. Lakini hakuna anayeweza kuja isipokuwa yeye amenipa mimi huyo tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu, hapa majina yao yalipowekwa kwenye kitabu cha uzima cha mwana kondoo”. Sio kwa kasisi wa mtaa wa kanisa bali kwenye kitabu cha uzima cha mwana – kondoo.

Lakini angalia Yesu alisema, ya kwamba katika wakati huu wa mwisho tena hizo roho mbili zingefanana tena sana. Hiyo ni kweli? Sasa angalia zitafanana sana kuliko hizo zilivyokuwa. Huu ni wakati wa mwisho loo, enyi watoto! Mungu na aturehemu! Mpaka, Hata ingefanana sana “ hata ingewapoteza hata kama yamkini walioteuliwa” sasa utalitambua je tulilitambua je katika siku hizo? Utalitambua je leo? Namna ile ile, dumu na Neno. “Yesu Kristo yeye yule jana, leo na hata milele”.

Sasa ujali ujumbe huu wote. Na unaposikiliza kanda, hata labda nitakuwa nimeondoka siku moja hapo Bwana atakapomaliza nami hapa duniani, mtarejea kwenye huu. Isikilizeni sauti yangu, yale ninayowaambia kama ikinichukua kabla ya kuja kwake, kumbukeni tu, nimenena nanyi katika jina la Bwana kwa Neno la Bwana Naam.

Sasa angalia wakati Musa aliposhuka kwenda Misri, akiwa na ujumbe wa BWANA ASEMA HIVI, naye alithibitishwa; akawaita Israeli, waliokuwa ni watu, si kanisa Israel walikuwa watu; hawakuwa kanisa kamwe maana, neno kanisa linamaanisha “waliotiwa mafuta chini ya Neno, halafu wakitwa, wake, wa kanisa la Mungu. Ndipo wakarudi nyuma, kwa maana hawakuamini Neno la Mungu, na wakamsikiliza nabii wa uongo natumaini hilo lina zama ndani.

Israel wakiwa watu wa Mungu waliotoka wakiwa chini ya mkono wa Mungu, wana upako wa Neno.....na nguvu za Mungu, wakaona ishara na maajabu ya Mungu. Na wakati Mungu alipokuwa akiendelea pamoja nao, nabii wa uongo akaingia, ametiwa mafuta, akawafundisha jambo fulani kinyume cha Neno la Mungu la asili waliokuwa wamesikia; kisha kila mmoja wao akaangamia jangwani ila watu wa tatu tu. Shikilieni jambo hilo.

Angalia si mayesu wa uongo. Makristo wa uongo wao wana amini wametiwa mafuta, bali wao wanajua wao si yesu. Manaona hilo ni

dhihiri sana kama mtu alipanda juu na kusema, leo hii, Angalia makovu kwenye mkono wangu. Angalia katika paji la uso wangu mimi ni Yesu “ Vema sasa tunajua jambo hilo si sahihi pia, kumbuka, Yesu hakusema kamwe ya kwamba jamaa hao wangetokea. Yeye alisema wakatokea “Makristo waongo” “makristo” wingi, madhehebu, na kadhalika, waliotiwa mafuta; waliotiwa mafuta kwa Roho wakimadhehebu wala si Neno. Mnalolifahamu? Si Yesu wa uongo mnaona? Loo ni dhahiri jinsi gani! Jinsi sisi.....Hakika hamtakosa hili!

Angalia kwenye siku za mwisho. “Hufanana sana ingewapoteza walioteuliwa kama yamkini” Loo Jamani! Sababu ya walioteuliwa kutopotezwa, mwajua ni kwa nini? Ni kwasababu wao ni Neno. Mwaona? Ni kama tu uhai uliokuwemo kwenye shina, nilisema muda mchache uliopita, huo hauwezi kujikana wenyewe mnaona, Huo ni Neno na katika majira ya Neno hiyo ni kweli sababu ya walioteuliwa, Yesu alisema hawatadanganywa ni kwa sababu wao ndio Neno hilo. Hawawezi kuwa kitu kingine hawawezi kusikia kitu kingine. Hawajui kitu kingine.

4

Nukuu za Kiingereza

“Wapakwa mafuta wakati wa siku za mwisho” Aya 23-28, 32-46, 57-60, 66-70, 88-102, 115, 132, 176, 182, 186/

“Mambo vile yatakavyokuwa” Aya 100-103, 113-116/ unyakuo Aya 143-149/

“Kristo akifunuliwa katika Neno lake mwenyewe” Aya 29-30/

“Kujaribu kumtendea Mungu kazi” (Kitabu cha 7 na 2) uongozi kitabu cha 7 na 7 aya 258 – 264.

Jiwe la kiroho la kujengea na. 117 kutoka kwenye Neno lililofunuliwa la saa hii, Yamekusanywa na Gerd Rodewald friedenstr. 69 D-75328 Schomberg, Germany Simu (+49) 72357613 Fax: (+49) 72353306

Anakuja mmoja na ujumbe ambao ni moja kwa moja ni Biblia na kazi ya haraka itazunguka dunia. Na mbegu zitaingia magazetini, vitu vya kusomea, mpaka kila mbegu iliyokusudiwa kimbele imesikia. (Ndugu Branham katika mwenendo utaratibu na mafundisho uk 724)

Kwa nakala zaidi za kiingereza au kiswahili Andika kwa:

Charles E. Y. Kanju,

Box 553 Korogwe - Tanga

E-mail: Chaelika@livel.com

Cellphone: 0784 704299/ 0718230098